JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA**

C©SOTA
COPYRIGHT OFFICE OF TANZANIA

# TAARIFA KWA UMMA

**UTAMBULISHO WA KAMPUNI MPYA YA KUKUSANYA NA KUGAWA MIRABAHA KWA KAZI ZA DARAJA LA VIELELEZO VYA KUSIKIA NA KUONA – "TANZANIA AUDIOVISUAL COLLECTION LIMITED" (TAVIC) NA KUHUISHWA KWA LESENI ZA KAMPUNI YA KUKUSANYA NA KUGAWA MIRABAHA KWA KAZI ZA DARAJA LA MUZIKI "SOCIETY OF MUSIC ADVOCACY LIMITED" (SOMA) NA KAMPUNI YA KAZI ZA DARAJA LA MAANDISHI "TANZANIA REPRODUCTION RIGHTS SOCIETY LIMITED (TANRRS)"**

Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) inapenda kufahamisha umma kuwa, kufuatia marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya Mwaka 1999 yaliyofanywa kupitia Sheria ya Fedha Na. 5 ya Mwaka 2022 na Kanuni za Hakimiliki na Hakishiriki (Ukusanyaji na Ugawaji wa Mirabaha) **(Kampuni za Kukusanya na Kugawa Mirabaha)**, za mwaka 2023 (Tangazo la Serikali Na. 211), misingi ya kisheria inaruhusu mashirika binafsi yanayoongozwa na wabunifu wenyewe kusimamia ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha.

Mnamo tarehe **27 Julai 2026**, COSOTA ilitoa leseni ya ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa **kampuni mpya** ya kazi za daraja la vielelezo vya kusikia na kuona ya **Tanzania Audiovisual Collection Limited (TAVIC)**.

Aidha, COSOTA **imehuisha** leseni za kampuni mbili kwa mujibu wa kanuni baada leseni za kampuni hizo kuisha muda wake wa mwaka mmoja. Kampuni hizo ni:-

1. **Society of Music Advocacy Limited (SOMA)**: Leseni yake **imehuishwa** kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa ajili ya ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kutokana na matumizi ya kibiashara ya **kazi za muziki**.
2. **Tanzania Reproduction Rights Society Limited (TANRRS)**: Leseni yake **imehuishwa** kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa ajili ya ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kutokana na matumizi ya kibiashara ya **kazi za maandishi**.

Majukumu ya kukusanya na kugawa mirabaha chini ya Kampuni hizi yataanza rasmi tarehe **1 Julai 2026, hadi 30 Juni 2027**.

COSOTA inaendelea kubaki na jukumu la kisheria la kusimamia utendaji kazi wa kampuni hizi katika ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha chini ya Kifungu cha 51 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki.

Aidha viwango vya tozo za ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha vinatakiwa kuandaliwa na kampuni zilizopewa leseni na kuwasilisha COSOTA kwa ajili ya kukaguliwa na kupitishwa kabla ya kuanza kutumika.

Kwa watumiaji wa kibiashara wa kazi za Muziki, Maandishi au Vielelezo vya Kusikia na Kuona (Audiovisual) wanatakiwa kisheria kulipia matumizi ya kazi hizo ili kuweza kupata leseni kutoka kwa kampuni zilizopewa dhamana ya usimamizi wa matumizi ya kazi hizo.

COSOTA inatoa wito kwa Wasanii wa Muziki, Waandishi wa Mashairi, Watayarishaji wa Muziki, Watayarishaji wa Filamu, Waandishi wa Miswada ya Filamu, Waandishi wa Vitabu na wadau wote wanaofanya ubunifu mbalimbali kulingana na madaraja hayo, kujiunga uanachama wa kampuni zilizopewa leseni ili waweze kunufaika zaidi na matumizi ya kazi hizo.

Kwa maelezo zaidi kuhusu usajili wa uanachama, ada za leseni au mahitaji ya nyaraka, tafadhali tembelea tovuti rasmi za Kampuni hizo au wasiliana na Shirikisho au Vyama husika au Ofisi za COSOTA.

**Imetolewa na:**

Ofisi ya Hakimiliki Tanzania – COSOTA

**07 Agosti 2026**

ORD258398